Uwe Na Hakika Na Mungu

Na inasomeka hivi:

Basi Elija, Mtibishi, wa. . .mwenyeji *wa Gileadi, akamwambia Ahabu, Kama BWANA, Mungu wa Israeli, aishivyo, ambaye ninasimama mbele zake, hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii mitatu ila kwa neno langu.*

Neno la Bwana likamjia, kusema,

Ondoka hapa, geuka, uende upande wa mashariki, ujifiche karibu na kijito cha Kedrithi—*Kerithi,*. . . (Nakusudia kusema). . .*kinachokabili Yordani.*

Itakuwa utakunywa maji ya kile kijito; nami nimewaamuru kunguru wakulishe. . .

Basi akaenda akafanya kama alivyosema BWANA; kwa kuwa akaenda karibu na kijito cha Kerithi, kinachokabili Yordani.

Kunguru wakamletea mkate na nyama asubuhi, na mkate na nyama jioni, akanywa maji ya kile kijito.

Ikawa, baada. . .*siku kupita, kile kijito kikakauka, kwa sababu mvua haikunya katika inchi.*

Neno la BWANA likamjia, kusema,

Ondoka, uende Sarepta, ulio mji wa Sidoni ukae huko. Tazama, nimemwagiza mwanamke mjane wa huko akulishe.

Basi, akaondoka, akaenda Sarepta; hata alipofika langoni pa mji, kumbe! mwanamke mjane alikuwa akiokota kuni, akamwita, akamwambia, Niletee, nakuomba, maji kidogo chomboni nipate kunywa.

Alipokuwa akienda kuleta, akamwita akasema, Niletee, nakuomba, kipande cha mkate mkononi mwako.

Naye akasema, Kama BWANA, Mungu wako, aishivyo, sina mkate, ila konzi ya unga katika pipa, na mafuta kidogo katika chupa; nami ninaokota kuni mbili ili niingie nijipatie nafsi yangu na mwanangu, tuule tukafe.

Eliya akamwambia, Usiogope; enenda ukafanye kama ulivyosema; lakini unifanyie kwanza mkate mdogo ukaniletee; kisha ujifanyie nafsi yako na. . .*mwanao.*

Kwa kuwa BWANA, Mungu wa Israeli, asema hivi: Lile pipa la unga halitapungua, wala ile chupa ya

mafuta haitaisha, hata siku ile BWANA atakapoleta mvua juu ya nchi.

LILE NENO LILILONENWA

Basi akaenda, akafanya kama alivyosema Eliya; na yeye mwenyewe, na Eliya, na nyumba yake, wakala siku nyingi.

Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta haikuisha, sawasawa na neno la BWANA lililonenwa na *kinywa cha Eliya.*

1 Kwa ajili ya mazungumzo ya asubuhi ya leo, kabla tu ya kwenda katika nchi za ng'ambo, nimelichagua somo hili: *Uwe na Hakika na Mungu.*

2 Na sasa, Bwana, libariki Neno Lako linapotangazwa, na Roho Mtakatifu ashike nia zetu na mawazo yetu, na atutayarishe kwa ajili ya kuzuru Kwake, kwa kuwa tumemuomba aje. Kwa kuwa hatuji katika nyumba ya Bwana tupate kuonekana ama kuona, bali kujifunza Kwako, na kujua tabia Yako, na njia Yako, na kusudi Zako, tupate kukabiliana na shida za maisha tukiwa na hakika halisi, tukiwa na hakika na Mungu. Tujalie, Bwana. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

3 Hapana shaka ilikuwa asubuhi ya kuogofya sana. Kulikuwa na joto sana na mavumbi, na watu walikuwa barabarani wakifa kwa njaa, na nchi ilikuwa na joto jingi sana hata ilikuwa tayari kuungua. Haya yote yalikuwa yakionyesha dhambi zao na utovu wao wa uadilifu.

4 Mwaona, Ahabu alikuwa akitawala katika—katika Israeli wakati huo—ama juu ya Israeli, naye ndiye aliyekuwa mbaya sana kati ya wafalme wa Israeli. Hapakuwepo na mfalme aliyekuwa mbaya kama Ahabu. Kwa kuwa yeye, kwa sababu alikuwa amefundishwa na kujua vizuri zaidi, hakuacha kuendelea kutomfurahisha Mungu katika kila kitu alichofanya. Ingawa alikuwa na taratibu kuu ya majeshi, na watu walikuwa wamefanikiwa sana chini ya utawala wake. . .Hata hivyo, huwezi kutokumpendeza Mungu na utarajie kuzidi kufanikiwa kwa muda mrefu sana.

5 Kisha, katika arusi yake, badala ya kuoa kati ya watu wake, aliendа zake akaoa mwenye dhambi, kafiri, mwabudu sanamu. Alimuoa Yezebeli. Naye hakuwa mwamini.

6 Na hamna mwamini anayepaswa kumwoa asiyeamini, kwa hali yo yote. Unapaswa kuoa aliye mwamini kila mara.

7 Bali Ahabu alikuwa ametenda jambo hili ovu. Na hapana shaka kwamba Yezebeli alikuwa mwanamke mrembo. Naye alivutiwa na urembo wake badala ya tabia yake. Hiyo ndiyo . . . Watu wengi sana hufanya kosa lilo hilo hata wakati wa leo.

8 Naye akaingiza ibada za sanamu katika taifa, kati ya watu. Nao hao watu, hao makuhani, wahudumu wao, walinaswa na haya matakwa makuu yaliyopendwa na watu.

9 Na ni picha kamili ya nchi yetu leo. Tumevutiwa na matakwa ya watu. Hapana shaka hao makuhani walidhani ni sawa mradi tu serikali yao iliruhusu hayo. Bali sijali serikali iliruhusu nini, inapaswa kuwa kile Mungu alichoruhusu. Nao watu wakadhani ingekuwa sawa kama walishiriki katika baadhi ya mambo yao ya kilimwengu.

10 Na huenda mtu akaniuliza nikanushe yale ambayo nimenena sasa hivi, ya kwamba ilikuwa picha halisi ya siku hizi. Huenda tusiwazie ya kwamba sisi ni waabudu sanamu, bali ndivyo tulivyo. Nayo serikali inatoa kibali chake. Watu siku hizi ni waabudu sanamu, kwa sababu wao—wao huabudu sanamu. Baadhi yao huabudu wachezaji wa sinema kama sanamu zao. Wengine huabudu fedha kama sanamu. Na wengine huabudu wachezaji wa televisheni kama sanamu. Bali yote unayoweka mbele ya Mungu ni sanamu, hata iwe nini.

11 Hata yule—Shetani, mshtaki wetu mkuu ni mjanja sana, hata wakati mwingine huliweka kanisa mbele ya Mungu. Huenda mkawa na kanisa kuu. Huenda likawa ni mjengo mzuri sana, ama huenda ikawa ni dhehebu kubwa sana, na tena, huenda ikawa ni kusanyiko kubwa, bali usiache cho chote kije mbele ya Mungu moyoni mwako. Chochote ndani—mbele za Mungu ni sanamu.

12 Na hawa watu walijua ya kwamba hawakuwa wa kiroho kama walivyokuwa chini ya tawala za wafalme wengine. Nao walidhani eti kwa sababu wao walikuwa taifa la kidini kwamba kila kitu kingekuwa sawa. Na hivyo ndivyo, tumefikia mahali hapo pia.

13 Miezi michache iliyopita nilikuwa nikizungumza na rafiki msiri wangu. Naye akasema, "Ndugu Branham, naamini ya kwamba wewe huilaumu hii Marekani sana." Akasema, "Daima unaikemea dhambi na jinsi Mungu ataliadhibu taifa hili."

14 Nikasema, "Hana budi kufanya. hivyo kusudi awe mwenye haki."

Akasema, "Lakini Ndugu Branham, unasahau ya kwamba taifa hili lilianzishwa juu ya Maandiko, na wazee wetu walikuja humu kisha Mungu alitupa huu urithi, nasi ni taifa la kidini."

15 Nikasema, "Hayo ni kweli, hayo yote. Na hamna anayejua jinsi ninavyolifurahia taifa hili. Bali tazama, ndugu yangu, Israeli pia ilichaguliwa na Mungu, na akawapelekea manabii na watu mashuhuri. Bali Mungu hawezi kuvumilia dhambi. Aliwafanya Waisraeli wavune kila punje waliyopanda. Na kama aliwafanya Waisraeli wavune walichopanda, atatufanya tuvune tunachopanda." Yeye hana upendeleo.

16 Nasi tumefikia mahali kuwazia ya kwamba eti kwa sababu tunategemea yale wazee wetu walifanya, ama juu ya yale ya waanzilishi wa makanisa yetu, jinsi walivyojitolea sana kwa Mungu—ambayo ni sawa na yanapendeza sana—bali hatuwezi kupata wokovu kwa yale waliyofanya! Wokovu ni jambo la kibinafsi kati ya kila mtu na Mungu. Si na taifa letu, na kanisa letu, bali sisi wenyewe mbele za Mungu tunajibu.

17 Imefikia mahali ambapo katika nchi yetu hata kati ya watu wa rohoni sana tulio nao . . . Unawaendea wanaume na wanawake wa rohoni, na kupata kwamba rohoni mwao mnakosa jambo fulani.

18 Tumekuwa . . . Katika majuma machache yaliyopita nimekuwa nikizungumzia baadhi ya mambo haya na kuona hayo katika watu niliowadhania ndio kiini, hata hivyo nikaona ya kwamba wao wanatilia mkazo mambo ya dunia hii, wakienda huku na huko wakisema, "Mungu hunipa ninino iliyo kubwa ya zote; Mungu hunipa . . . " Unadanganya!

19 Mambo makuu ya anasa hayawi katika mapenzi ya Mungu daima. Mungu huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. Lakini kile ulimwengu unachohitaji leo si imani ya ulaghai, kujaribu kujidanganya mwenyewe kwa jambo fulani na kuliita la kiroho . . .

20 Wakati mwingine imani itatenda miujiza mikuu na hata hivyo haitoki katika moyo wa kiroho. Je! Bwana wetu hakusema, "Wengi watanijia siku ile na kusema, 'Sikufanya *hili* na *lile* katika Jina Lako?' Nami nitakiri mbele zao, ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu." Je, uovu ni nini? Ni jambo unalojua kufanya sawa na hulifanyi. "Sikuwajua ninyi kamwe," Yeye atasema. Nasi tunaishi katika siku hiyo.

21 Tunachohitaji leo si vitu vingi vya anasa; tunavyo. Hatuhitaji makanisa makubwa; hatuhitaji kusanyiko kubwa. Hatuhitaji mengi zaidi katika redio na televisheni. Hatuhitaji mengi zaidi ya mambo haya. Bali tunachohitaji leo ni kuwa watu wa rohoni, ni watu ambao watajinyenyekeza mbele za Mungu hata ingawa hawana hela, nao wataomba hata roho aliye ndani yao ameridhishwa na uzuri wa Mungu, na ufufuo utendeke humo ndani ya mioyo yao ambao hugeuza misimamo yao na hali wanayoishi kwayo.

22 Huenda usiwe na jozi la viatu miguuni mwako. Huenda umevaa nguo zilizochakaa, lakini mna kitu moyoni mwako kinachomwimbia Mungu nyimbo. Afadhali nipate hicho kuliko fedha zote ulimwenguni.

23 Kwa hivyo huwezi ukasema ya kwamba mambo ya kawaida kila mara ni ishara ya baraka Zake Mungu. Daudi alinena hayo kwa Mungu, ya kwamba alikuwa amemwona aliye mwovu akitandaza yake—kama mti mkubwa wa Ulaya. Bali Mungu akamuuliza, "Je, umekwisha fikiria mwisho wake?" Haidhuru

tunavaa nguo nzuri jinsi gani, inatupasa kula chakula kiasi gani, hayo siyo yanayoenda mbele za Mungu. Mwili huu tunaoishi ndani yake huangamia si hoja unaushughulikia jinsi gani. Bali ni nafsi iliyo katika mwanadamu; ni hali ya roho inayoenda katika uwepo wa Mungu Aliye Hai.

24 Bali sisi huchukua mambo bila kufikiria. Tunafikiri ya kwamba eti kwa sababu tu sisi ni taifa . . . Vivyo hivyo Ahabu na Israeli wote siku hiyo walikuwa wamechukua mambo bila kufikiria, ya kwamba kila kitu kilikuwa sawa. Makuhani wao na wahubiri wao walikuwa wamejaribu kuwaambia, "Mambo yote ni shwari, kila kitu ni sawa." Bali walikuwa na mmoja; huyo alikemea mambo mabaya, kwa sababu huyu mmoja alijua ya kwamba Mungu mtakatifu hangaliridhishwa na mwenendo wa kisasa wa dini isiyo takatifu . . .

25 Vivyo hivyo Mungu wa Mbinguni hudumu vivyo hivyo leo. Na jitihada zetu zote na mambo makuu ambayo tunajaribu kufanya, Mungu hatafurahishwa nje ya maisha yaliyotakaswa mbele Zake.

26 Huenda tukajenga mashule, na madhabahu, na maskani; huenda tukawa na vyama, huenda tukafanya mambo makuu, hata hivyo Mungu hataridhika hata nafsi ya mwanadamu itakapokuwa imetakaswa . . . juu ya madhabahu ya Mungu, imewekwa wakfu kwa ajili ya kazi za Mungu. Na hupati hayo tena.

27 Utaona kwamba mikutano yetu ya maombi ni hafifu sana, yapata dakika moja tu ya maombi, tukaruka kitandani. Tunaona ya kwamba hayo hutendeka mara moja ama mbili kwa siku. Wakati sisi sote tuna hatia! Uadilifu wa taifa letu unaoza. Tuna akina Billy Graham na akina Oral Roberts kila mahali, bali mpaka kiu kitakapoingia katika moyo wa Amerika kuirudisha kwa Mungu Aliye Hai tena, kwenye tukio lililo hai, hata kufikia imani isiyokufa katika Mungu Aliye Hai, tunavuruga tu akili zetu, kama wasemavyo, kabisa.

28 Huenda tukatembea vifua mbele, huku tumeugeuza kala zetu nyuma, na kutembea barabarani na kupenda kuitwa daktari au kasisi. Tunaweza kuwa wachungaji wa makanisa yaliyo makubwa sana nchini, na huenda tukawa watawa tuwezavyo kuwa, hata pasiwepo mtu anayeweza kuyaelekezea maisha yetu kidole. Bali mpaka hiyo nafsi iliyo ndani mwetu iwake moto kwa ajili ya Mungu, hata kitu fulani humo ndani kimwonee shauku: "Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu" . . . Hata tutakapopata tukio la jinsi hiyo.

29 Kwa hivyo, Ukomunisti na kadhalika utafanikiwa kama wanavyofanya, na kujiunga kwote ambako tunaweza kufanya hakutaukomesha kamwe. Umebashiriwa kuja. Lakini Mungu analiita Kanisa Lake.

30 Jinsi mwanamke huyu hapana budi alikuwa kama Eliya, kwa sababu kwa kawaida matendo yako huonyesha wewe ni nani. Na tena, alikuwa amechaguliwa kumkaribisha nabii wa Mungu. Kumbuka, alikuwa Mtaifa, si Myahudi.

31 Na hiyo nchi ilikuwa inaungua. Na hapana shaka maskini mwanamke huyo, akiwa mtu wa namna hiyo, akiwa wa namna ya mwamini. . . Kwa kuwa tunaona ya kwamba Mungu hangalimwita, kama hangalikuwa mtu aliyestahili kumkaribisha nabii wa Mungu. Kwa kuwa hangalimtuma nabii Wake aende katika nyumba isiyostahili.

32 Haikuwa chagua lake, lilikuwa changua la Mungu. Si mwanamke aliyemwagiza, ni Mungu aliyemwagiza. Alikuwa amewekwa karibu na kijito; ndege walikuwa wakimlisha. Bali lilikuwa agizo la Mungu kwa jambo fulani kutendeka. Naye Mungu hakika alikwenda kwa mwamini aliyekuwa na tabia ya Eliya.

33 Alikuwa mwanamke mjane. Nasi sote tunajua yale ambayo yeye—mwanamke mjane angalipitia, huku mumewe amekufa na ana kijana mvulana wa kulea.

34 Na humo nchini wao walitegemea mimea yao. Hawakuwa na miradi kama tulivyo nayo leo na—na viwanda vya ulinzi. Wao walitegemea mimea yao. Na kwa kuwa uovu wa watu na utovu wao wa uadilifu ulikuwa umesababisha ukame nchini, hapa wao wote walikuwa wakiteseka kwa njaa na kufariki.

35 Kisha tunaona ya kwamba hapana shaka yeye alikuwa ameomba usiku baada ya usiku usiku kucha, alipoanza kuona lile pipa la unga likipunguka zaidi na zaidi na zaidi. Na hapana shaka ilifikia wakati hata hapakuwepo na kikombe kingine cha unga katika hilo pipa. Yote aliyokuwa nayo ni konzi dogo sana. Mauti yalikuwa yanaingia moja kwa moja mlangoni mwake. Kwa kuwa hapakuwepo na njia ya kuupata mwingine. Taifa zima lilikuwa linaumia kwa njaa.

36 Na mafuta yalikuwa, ni kijiko kidogo tu kilichobaki mle kwenye chupa. Ni mafuta kiasi hiki tu na unga kiasi hiki vilivyosimama kati yake na mauti. Hapana shaka alikuwa mwaminifu sana katika maombi yake. Hebu hilo liguse nyumba yako; utakuwa mwaminifu zaidi kuliko tulivyo asubuhi ya leo. Tunapojua ya kwamba mauti yapo mlangoni.

37 Nami naamini labda tungefikiria hili; ya kwamba alikuwa ameomba usiku kucha, kwa kuwa siku moja zaidi ingalimaliza mambo. Angaliangalia midomo iliyokauka ya mvulana wake mdogo mwenye umri wa miaka mitatu minne, naye angeona mifupa yake binafsi ikipungua huku nyama zikiitoka. Na bila shaka lilikuwa jambo la kuchukiza sana huku huyu mama, akiona mambo haya yakiendelea, na bado mikono yake ikiwa mbele za Mungu akiomba mchana na usiku. "Sasa, tumefikia konzi moja ya unga na kijiko kimoja cha mafuta."

38 Mwajua, ni jambo la ajabu. Mungu na aruhusu hili likolee ndani ya kila mmoja wenu kama hamtanisikia nikihubiri tena. Hebu huu na uwe ujumbe. Ni ajabu, ajabu sana, kwamba Mungu wakati mwingine hutenda mambo hivyo.

39 Mnajua, baada ya sisi kukiri dhambi zetu na kutimiza kila sharti analohitaji Mungu . . . Tumemwamini Mungu. Kuna hali ya mambo ambayo sharti itimizwe, na ni kulingana na mapenzi Yake. Nasi tumekwisha kukiri dhambi zetu, na tumesahihisha mambo yote tuliyoyatenda, tukafanya yote tunayojua kufanya, kila sharti ambalo Mungu ameamuru au kuagiza, tumetimiza masharti hayo, hata hivyo Yeye yu kimya; hatujibu . . .

40 Nina hakika ya kwamba ninawazungumzia watu asubuhi ya leo ambao wamepafikia mahali hapo. Nimekuwa hapo mara nyingi mimi mwenyewe. Ambapo nimerudi nyuma na kuyafuatilia maisha yangu na kupindua kila jiwe, nami ningeona ya kwamba nilifanya kosa, ningelitubu na kusema, "Bwana Mungu, nitalisahihisha," na kuenda kufanya hivyo. Kisha narudi tena na kusema, "Sasa, Bwana, Wewe ni Mungu; utanijibu. Kwa kweli nimetimiza kila sharti ulilotaka mimi nitende. Na kila sharti, nimelitimiza." Na hata hivyo hatatenda neno, yaonekana yu kimya; hapo ndipo inakupasa kuwa na hakika ya kwamba Yeye ni Mungu. Usife moyo; jambo pekee ni kwamba, ya kwamba moyoni mwako uwe na hakika na Mungu.

41 Somo langu, kuwa na hakika kwanza kabla haujatenda lo lote; uwe na hakika moyoni mwako ya kwamba ni Mungu. Na utakapotimiza kila kitu alichosema, kisha una hakika ya kwamba Yeye ni Mungu, hapo ndipo imani inapoanza kutenda kazi, papo hapo. Imani inasimama imara, kwa kuwa inajua ya kwamba Yeye yuko.

42 Nawe umetimiza kila sharti. Unaamini ya kwamba Yeye yuko, na imani inashikilia imara. Lo, Jina Lake libarikiwe. Imani haitasogea, kwa sababu ina hakika ya kwamba Mungu yuko naye huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii.

43 Hebu hili liingie kwenye kilindi kabisa na lisiondoke kwenu, enyi Maskani ya Branham. Iwapo umetimiza masharti ya Mungu, na moyoni mwako unaamini ya kwamba Yeye yuko, Mungu anaijaribu imani yako tu, kwa sababu Yeye hupenda kufanya hivyo. Umekiri dhambi zako na umetimiza kila sharti ambalo Mungu anahitaji, na hata hivyo Yeye ananyamaza kimya, kumbuka, imani inasema ya kwamba Yeye yuko. Basi imani inashikilia hilo, bila kujua maana yake, bali inajua ya kwamba Yeye yuko, na ina hakika ya kwamba Yeye yuko.

44 Basi kumbuka, kama Yeye yuko, maneno Yake hayana budi kuwa kweli. Na iwapo alikutaka ukabiliane na hali hii ya mambo na umeikabili, Yeye hana budi kujali Neno Lake. Usirudi nyuma, na kusema, "Mimi sikuponywa. Mimi . . ." Lo, ewe maskini, mwenye imani dhaifu. Usiamini hilo. Kama kila kitu tayari

kimetubiwa, na kila kitu kiko nje, nawe umetimiza masharti ya Mungu, imani inashikilia papo hapo. Hamna kitu kinachoweza kuitikisa. Yeye yuko, nawe una hakika. "Wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa za tai. Watapiga mbio, wala hawatachoka; kama watakwenda kwa miguu, hawatazimia."

45 Ngoja, utakapotimiza masharti Yake; hiyo inaileta imani yako kwenye kuonyesha nguvu dhahiri. Kama umekwisha timiza...Masharti ya Mungu yamekwisha kufanywa—ama kutimizwa, na umekwisha kuyafikiria kabisa, na umefanya kila kitu ambacho Mungu alikutaka ufanye, basi imani yako inatulia papo hapo ya kwamba Yeye yuko. Uwe na Hakika na Mungu!

46 Mnajua, Yeye anapenda kutujaribu. Yeye hupenda kuona imani yako itakavyofanya. Ulijua hilo? Mungu hupenda kuona vile utakavyofanya. Unaposema, "Ee Bwana, nakuamini; Wewe ni Mwokozi wangu. Ninaamini ya kwamba Wewe ni Mponyaji; naamini Wewe ndiwe unayetoa Roho Mtakatifu; na mambo ninayohitaji, Wewe ni Mungu anayetoa hayo!"... Kisha basi ukitubu dhambi zako zote na kumuahidi Mungu yale utakayotenda iwapo atakupa afya, kisha kwa sababu haitendeki, unakimbia kama mwoga mahali fulani, Mungu hawezi kutumia hiyo. Hamna njia Kwake kukutumia. Hamna njia Kwake kukujibu, kwa sababu Yeye hujibu tu kwa imani. Kisha kwa gafla unaondoka naye hawezi kujibu. Bali imani iliyo halisi na ya kweli hutulia hapo, ikiwa na hakika ya kwamba Yeye ni Mungu. Ni hakika ya kwamba Yeye yuko.

47 Na kama Mungu akiagiza jambo hili litendwe, kukiri dhambi zako na kadhalika, na umekwisha kufanya hivyo, imani inasema ya kwamba Yeye yuko; ni hakika kwamba itatendeka. Haja yako lazima itimizwe. Lo, na—natumaini hamtakosa hilo. Kama una hakika na Mungu, Mungu ana hakika na Neno Lake. Yeye anangojea tu kukujaribu.

48 Alifanya hivyo mara nyingi. Hebu tusimulie kisa kimoja au viwili. Hebu tuchukue habari za wale wana wa Kiebrania. Haikuwapasa kuzisujudu sanamu. Mungu alikuwa na matumaini kwao. Nao waliposikia wangeenda kwenye ile tanuru ya moto, wao walisema, "Mungu wetu anaweza kutuokoa na hii tanuru. Bali kama hatafanya hivyo, sisi hatutaisujudia yo yote ya sanamu zako." Mnaona, wao walikuwa na yakini na hakika na Mungu.

49 Wao walijua ya kwamba Yeye alikuwa Yehova. Wao walijua ya kwamba Yeye huyajibu maombi. Bali kama aliwafanyia hivyo au la, ingekuwa yenye manufaa, kwa hivyo wao wakatoa tamshi lao, wakakiri dhambi zao, kisha wakatembea wakielekea mautini.

50 Walipokuwa wakielekea kwenye ile tanuru iliyowaka moto, wakijua kwamba walikuwa na hakika ya kwamba kama Mungu

akiwaachilia wachomwe moto, Yeye angewafufua tena katika ule ufufuo . . . Wao walikuwa wana hakika na Mungu, kwa kuwa walijua ya kwamba Mungu angetenda kila kitu kwa manufaa yao. Na tunapokuwa na hakika na Mungu, tunajua Mungu hutenda kila jambo kwa manufaa yetu.

51 Kwa hivyo wakatoa tamshi moja. Wao walikuwa na hakika. Na wakaingia moja kwa moja katika tanuru iliyowaka moto, na Mungu akawaacha waingie mle, huku ameketi akiwaangalia. Alitaka kuona watakalofanya.

52 Mfalme aliposema, "Je, mlisujudu tarumbeta ilipolia?" wao walisema, "La, hatukusujudu." Ndiyo hiyo imani yako, ikishikilia imara kabisa.

"Vema, basi kama hamkusujudu, mnajua amri yangu?"

"Ndio, tunajua amri yako."

"Amri yangu ni kwamba ile tanuru itatiwa moto mara saba kuliko ilivyopata kuwa, nami nitawatupeni mle ndani. Je, sasa mnataka kusujudu?"

"La, hatutasujudu." Ndiyo hiyo imani yao.

53 Mungu alisema, "Vema, nitaona watakachofanya juu yake. Nitaona imani yao itakavyotenda."

54 Kwa hivyo akasema, "Ifungeni mikono yao, kisha mkaifunge miguu yao, halafu muwapeleke kwenye ile tanuru." Nao wakaenda kwenye hiyo tanuru huku moto uko mbele ya macho yao, huku Mungu amesimama akiiangalia. Bali wao walikuwa na hakika ya kwamba Yeye alikuwa Mungu. Wao walikuwa wamekwishaungama. Walikuwa wametetengeneza kila jambo walilojua. Walikuwa na hakika ya kwamba Yeye alikuwa Mungu.

55 Hivyo basi wakaenda moja kwa moja hata kwenye hiyo tanuru iliyowaka moto. Na mara katika dakika ya mwisho, ndiye huyu anashuka chini kutoka mbinguni katika gari la upepo, akaipeperushia mbali nao hiyo miali ya moto huku akiwafariji na kuwazungumzia.

56 Mungu huiachilia imani yako ifikie mahali ambapo itatenda jambo.

57 Kulikuweko na Ayubu wa Agano la Kale, wakati Shetani, mshtaki wetu, alimshtaki eti yeye hutenda dhambi kisiri. Bali Ayubu alijua hakuwa ametenda dhambi. Alijua ya kwamba tayari alikuwa ametubu kila kitu alichokuwa ametenda na akaweka sadaka ya kuteketezwa kule nje. Hayo ndiyo yalikuwa masharti ya Mungu. Hayo tu ndiyo Mungu aliyohitaji ilikuwa hiyo sadaka ya kuteketezwa pamoja na kuungama. Naye Ayubu aliisha fanya mambo hayo.

58 Kisha Shetani akasema, "Nitachukua ngamia zake, kwa kuwa yeye ni tajiri, nitazitwaa kondoo zake." Hatimaye akawatwaa watoto wake, aliokuwa amewapenda sana.

59 Bali hata hivyo Ayubu akasimama imara, kwa kuwa alijua ya kwamba Mungu. . .Vema, alikuwa na hakika Yeye alikuwa Mungu, kwa kuwa alikuwa amenena Naye, naye alikuwa ametimiliza masharti Yake. Yeye alitafuta-tafuta hata akaona, "Nimetoa kila sadaka ya kuteketezwa. Nilisema moyoni mwangu, 'Labda wakati watoto wangu walifanya ka—karamu na binti zangu wakahudhuria, labda huenda ikawa walitenda dhambi kisiri mioyoni mwao, kwa hivyo nitatoa sadaka ya kuteketezwa kutoka kwao na kutubu makosa yao.'"

60 Ee Mungu, mtu anapotimiza yale Mungu aliyosema yafanywe, yeye ana hakika Yeye ni Mungu; Yeye hana budi kujibu. Imani humwita ajitokeze kila mara.

61 Ukisha kufanya unayojua ni kweli, ukisha timiza masharti Yake, ukisha tubu na kusahihisha na kuyalipia, na kuyaweka mbele za Mungu, sijali amenyamaza vipi, Yeye yungali Mungu, akingoja kuiweka hiyo imani pale. Umetenda kazi zako, sasa Yeye anataka kuona imani yako kwa kazi zako. Anataka kuona utakachofanya.

62 Iwapo umekwisha kutiwa mafuta na kuombewa, Mungu anangoja aone utaaminije juu yake, si kukimbia kule Jumapili ijayo, na kupiga mbio kesho yake kwenda kwa mponyaji mwingine anayeuzuru mji; Yeye anangojea aone itakavyofanya imani yako, si kurudi siku inayofuata na kusema, "Najisikia vibaya sana; sidhani niliponywa." Wewe hustahili kuwa katika mstari wa maombi kwanza. Hauko—hauko—hauko tayari bado. Huamini ya kwamba Yeye ni Mungu. Mimi si . . .

63 Huenda ukasema, "Ndugu Branham, sikubaliani nawe." Matendo yako yathibitisha kile ulicho. "Kwa matunda yao mtawatambua." Kama mtu akisema yeye ni Mkristo, naye bado anakunywa pombe, anavuta sigara, anacheza karata, na anafanya mizaha michafu, kisha anasema sehemu ya Biblia ni kweli na sehemu yake si kweli. . .Huenda akaihubiri Injili, kisha anakana sehemu ya Biblia; yeye angali mwenye dhambi. Hajakuwa sawa bado.

64 Bali unapokiri waziwazi ya kwamba Mungu ni Mungu yule yule, na maisha yako yamewekwa mikononi Mwake kuwa, "Bwana, mimi ni udongo; Wewe ndiwe Mfinyanzi," basi omba utakalo. Imani haitatikisika kamwe; itasimama papo hapo.

65 Hata ingawa hali ya mambo itaonekana kama inaangukia kulia hadi kushoto, bali imani hiyo haitikisiki kamwe, kwa kuwa una hakika ya kwamba Yeye ni Mungu. Na iwapo Yeye yu Mungu, Yeye hutimiza ahadi Yake. Hawezi akafanya ahadi kisha akaivunja. Iwapo Yeye ni Mungu, hana budi kutimiza ahadi Yake. Lo, napenda hilo. Hana budi kudumu nayo.

66 Ayubu alitoa sadaka yake; alitenda kila kitu. Alijua ya kwamba alikuwa sahihi. Halafu hapo wakaja washiriki wa kanisa, baadhi ya makanisa ya madhehebu mengine, kasema,

"Ayubu, afadhali basi ukiri ya kwamba wewe ni mwenye dhambi, kwa kuwa Mungu hangalikuruhusu uadhibiwe hivi isipokuwa ulikuwa mwenye dhambi."

67 Bali Ayubu alisema, "Nimetubu dhambi zangu. Nimeishaweka dhabihu ya kuteketezwa mbele za Mungu, nami si mwenye dhambi." Yeye alijua alikokuwa amesimama. Basi kila kitu kikaendelea, kikaendelea na kuendelea na kuendelea, upesi ilivyowezekana, wakijaribu kumshusha moyo Ayubu na kumfikisha Ayubu mahali ambapo angemkana Mungu na kuikana ile sadaka ya kuteketezwa. Dakika ile ile unapochukulia hatua cho chote ulichotubu, inaonyesha udhaifu wako, kumshuku kwako Mungu. Ukimuomba Mungu jambo fulani kisha uondoke uende ukilishuku, basi wewe ni asiyesadiki wala si mwamini.

68 Ayubu alijua alikosimama, naye akasimama imara katika huo msingi.

69 Si ajabu Pruitt alisema katika saa yake ya kufa,

> Kwake Yesu nasimama;
> Ndiye mwamba ni salama.

70 Juu ya huo mwamba wenye imara wa kukiri kwa Ayubu. . .Hata mpenzi mkewe alimwacha. Wakati afya yake ilipokuwa imedidimia, na mwili ulikuwa majipu matupu, naye akajikwaruza-kwaruza na kuilaani siku aliyozaliwa, kasema, "Jua na lisiiangaze; mwezi usichomoze usiku."

Mkewe akasema, "Ayubu, wewe ni mwenye mashaka sana; mbona usimkufuru Mungu, ukafe."

71 Akasema, "Wewe wanena kama hao wanawake wapumbavu." Yeye alikuwa na hakika ya kwamba Mungu alikuwepo, naye tayari alikuwa ametimiza masharti. Lo, najisikia mtauwa. Yeye alijua alikuwa ametimiza masharti ya Mungu, na hilo lilitosha. Mungu alikuwa akijaribu imani yake. Ataijaribu yako; ataijaribu yangu.

72 Bali tunapoyatimiza masharti Yake, "Tubuni kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu," hiyo ni ahadi Yake. "Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? na awaite wazee wa kanisa; na wampake mafuta na kuwaombea. Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule na Mungu atamwinua." Hilo latosha. "Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi na kuombeana."

73 Umetimiza masharti ya Mungu, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Katika Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; wakishika nyoka ama kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru; kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hilo latosha.

74 Uwe na hakika na Mungu. Hakikisha moyoni mwako ya kwamba unaamini ya kwamba hilo ni Neno la Mungu. Ayubu alihakikisha.

Mkewe akasema, "Mbona usimkufuru ukafe. Kwani, unazidi kuwa mgonjwa wakati wote."

75 Jinsi Shetani hupenda kukutupia hilo. "Kwani, hujapata nafuu tangu ulipopakwa mafuta. Hujapata nafuu tangu hao wahubiri walipokuombea. Kwanza hao wahubiri hawako sahihi." Si juu ya huyo mhubiri; imani yako katika Mungu Aliye Hai ndilo jambo muhimu. . . Si kile mhubiri alicho, ni Mungu alicho. Mhubiri hakutoa ahadi; Mungu ndiye aliyetoa ahadi. Si juu ya mhubiri; ni juu ya Mungu na imani yako kuamini ya kwamba Yeye ni Mungu. Kwa hivyo uwe na hakika na Mungu. Uwe na hakika ya kwamba ni Mungu, na hilo ni Neno la Mungu, na Mungu yumo katika Neno Lake.

76 Kisha Ayubu akasema, "Wewe unanena kama mwanamke mpumbavu." Kasema, "Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; jina la Bwana libarikiwe." Yeye alikuwa na hakika ya kwamba Mungu alikuweko.

77 Na aliponena hayo kwa kinywa chake, ngurumo zikaanza kunguruma na umeme ukaanza kumemeta; Mungu akajitokeza; hilo daima humfanya ajitokeze jukwaani. Yeye hukaa kimya kwa muda mrefu.

78 Hivyo ndivyo anavyofanya, akikiangalia kikundi hiki cha Waamerika wanaoelekea jehanamu, wanafiki wanaohudhuria kanisa. Mimi sina hasira, bali dhambi humchukiza mtu ye yote aliye sawa mbele za Mungu. Sina hasira na taifa, sina hasira na watu, bali nina hasira na ibilisi ambaye amesababisha mambo haya kusudi awapofushe watu.

79 Hawa wachungaji vipofu pamoja na wahubiri wanawaacha waendelee na namna fulani ya theologia dogo zilizotengenezwa na wanadamu. Huna budi kuzaliwa mara ya pili, naye Mungu hutimiza Neno Lake. Kumwona Yeye anapowaita. Yakupasa kuwa na hakika ya kwamba Mungu yuko. "Wenye mfano wa utauwa, kisha wanakana nguvu zake . . . "

80 Huyu mwanamke mdogo maskini, yeye alijua ya kwamba Yeye alikuwa Mungu. Wakati hilo pipa lilipungua, na kupungua, na kupungua, na kupungua, hali ya mambo ikazidi kuwa mbaya na mbaya wakati wote. Bali Mungu alikuwa akiiachilia iwe hivyo. Yeye hupenda kufanya hivyo. Yeye hupenda kuijaribu imani yako kuona jinsi unavyoweza kutenda nayo, anakuacha upakwe mafuta na kuombewa, kisha anakufanya uugue zaidi, kasema "Haya njoo, Shetani, mjaribu; najua ya kwamba yeye ananiamini Mimi." Mungu abarikiwe milele! Lo, jamani! "Mjaribu sasa; najua aliamini Neno Langu kwa ajili yake." Je, Yeye angeweza kusema hilo juu yako?

81 Alisema hilo juu ya Ayubu, kasema, “Mfanyie lo lote unalotaka, bali usiutwae uhai wake, kwa kuwa najua yeye ananipenda. Amenitolea sadaka ya kuteketezwa; ametimiza masharti; alitenda niliyomwagiza kutenda, naye analiamini. Sasa, mviringishe juu ya makaa ya moto ukitaka.” Akatwaa kila kitu kutoka kwake; Mungu alivifanya maradufu alipomrudishia. Bila shaka atafanya hivyo!

82 Yeye huijaribu imani yetu kuona kama kweli tunaamini kweli ya kwamba Yeye ni Mungu.

83 Maskini mwanamke huyo hapana shaka alisema, “Niliomba; niliomba; najua ya kwamba mimi ni mtu wa Mataifa asiyestahili.”

84 Kumbuka, Yesu alinena habari zake katika Biblia; akasema, “Je, hakukuweko wajane wengi katika siku za Eliya? Bali yeye alipelekwa tu kwa mmoja, naye alikuwa mtu wa Mataifa.”

85 Lo yeye akasema, “Niliomba.” Na labda alipoona huo mkate mdogo wa mwisho, mauti tayari yalikuwa yameingia langoni na kuingia mlangoni. Kila mmoja apate mego moja, naye pamoja na mwanawe wafe. Naweza kumwona akiomba usiku kucha, huku upepo wenye joto unavuma, na nchi imekauka kabisa, watu wakilia na kupaza sauti kwa hofu mitaani. Akatembea huku na huko nyumbani. Akamtazama mvulana wake mdogo. Akazitazama nguo zake ndogo za kulalia, zote zilikuwa zimechakaa, huku miguu yake ikitokeza nje, akaitazama mikono yake, ina makunyanzi. Akatembea huku na huko, bali akasema, “Najua ya kwamba Yeye ni Mungu. Nimekwisha kuungama kabisa; nimetenda kila alichohitaji; nami naomba uhai wetu kwa ajili ya utukufu Wake.” Mungu akamwona.

86 Wengine wote walikuwa wakienda na kusokata rumba mahali fulani, wakijirembesha, wakiwa na maonyesho ya kisasa ya televisheni ama jambo fulani, wakiendelea tu na shughuli za ulimwengu. Bali mwanamke huyo alikuwa peke yake na Mungu.

87 Kukapambazuka. Akasema, “Maskini mtoto huyo alilia usiku kucha apate chakula; nitafanyaje na konzi moja ndogo ya unga?”

88 Mwajua, unga huo ulikuwa Kristo. Mwanafunzi ye yote wa Biblia anajua ya kwamba Kristo alikuwa ndiye Sadaka ya Unga. Na sadaka hiyo ya unga ilipaswa kusagwa na jiwe maalum pia, hata likakata kila chembe ndogo ya mahindi sawa, kwa maana Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na kila mwamini huamini hilo na kutulia juu yake. Haleluya! Unaweza kuchukua dini yako yote ya kale, iliyo baridi na ya kawaida unayotaka. Kwangu mimi naamini Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nachukua msimamo wangu katika ulimwengu wa makafiri. Ningali ninaamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

89 Hayo mawe yalikata kila chembe chake sawa sawa, kwa sababu Yeye ni yeye yule. Yeye ni Mungu yule yule aliyekuwa wakati huo, ndivyo alivyo sasa hivi, asubuhi hii. Daima atakuwa vivyo hivyo. Hiyo ndiyo maana ya unga huo.

90 Yale Mafuta maana yake ni Roho, kama tujuavyo kulingana na Ezekieli 4 na kadhalika. Hiyo ndiyo sababu sisi hupaka mafuta; ni Roho. Ni nini? Kama Yohana Mt. 4: "Baba anawatafuta hao wamwabudu katika Roho na Kweli." Yesu alikuwa ile Kweli. Alikuwa Sadaka ya Unga, na Mafuta haya yalikuwa Roho. Na Roho akichanganywa na ile Kweli hana budi kuleta kitu fulani. Ziweke pamoja, hizo hufanyiza mkate.

91 Lo, i wapi imani yenu? Wakati Neno la Mungu linapohubiriwa katika urahisi Wake, ingawa katika nguvu Zake ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, nalo Neno linatangazwa kwa ajili ya ule Unga, una yale Mafuta kuyachanganya na Unga. Huenda ikawa ni konzi ndogo au kijiko kimoja, lakini hata iwe nini, ni halisi.

92 Sasa, iko tayari kwa ajili gani? Iko tayari kwa ajili ya Msalaba. Iko tayari kwa kujitolea mwenyewe. Hilo ndilo linalokupasa kufanya. Kama Neno limekwisha kuhubiriwa, nawe una Roho ndani yake zikichanganywa pamoja, ni kujitolea kibinafsi kukanusha kila uchungu, kukanusha kila ugonjwa, kukanusha kila kitu kilicho kinyume cha Neno la Mungu na kusimama juu yake.

93 Daktari anasema *hili, lile,* ama *linginelo;* hilo halileti tofauti kamwe. Wewe unasimama nalo, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Unga huja; unapata Mafuta; unavichanganya.

94 Sasa, nasikia sauti. Ni punde tu baada ya mapambazuko. Sauti inanena na kusema, "Ondoka uende uwanjani ukaokote vijiti viwili." Uliona kwamba Maandiko yalisema vijiti viwili? Msalaba. Yeye ana unga na mafuta, lakini sasa ataitwa kutenda sasa, kutenda nayo. Haidhuru una kiasi gani, kiasi cha Unga ama Mafuta unayohitaji, bali huna budi kutenda—kujitolea mwenyewe, vijiti viwili.

95 Zamani za kale hawakupata njia bora zaidi ya kuwasha moto. Unapochukua kijiti na kukikingamisha kijiti kingine, na kuviwasha katikati, unachoma pande zote. Wahindi waliwasha mioto yao. Nimewasha moto mara nyingi usiku kucha, ninachukua gogo na kulilaza *hivi* na lingine *vile,* na kuendelea kulisukumiza motoni huku linawaka moto.

96 Kijiti hicho kilikuwa msalaba. Biblia ilisema vijiti viwili. Ile sauti ikanena, "Enenda huko uwanjani ukaokote vijiti viwili." Wakati uo huo huko mlimani kulikuwa na sauti iliyomngurumia yule nabii ikasema, "Shuka uende mjini; nimemwagiza . . . " Lo, jamani! Wote wawili walitii. Jambo fulani lazima litendeke. Wote wawili walitii.

97 Kama mhubiri akihubiri Neno, na yule mtu anayelipokea analiamini na kulitenda, jambo fulani halina budi kutendeka. Kama wewe ni mwenye dhambi, huna budi kuokolewa. Iwapo wewe ni mgonjwa, huna budi kuponywa, kwa sababu Mungu aliliahidi kama sisi tuna hakika na Mungu.

98 Bila shaka kwa vile Yeye ni Mungu, hana budi kutimiza Neno Lake. Bila shaka! Ndipo agizo lilikuwa, "Ondoka uende mjini, kwa kuwa nimemwagiza mwanamke mjane . . ." Ono likatokea mbele za nabii. Ndiye huyu hapa anakuja, akitembea. Hajui anakoenda; haileti tofauti. Yeye anatii tu.

99 Hajui vijiti vitakuwa wapi, bali mna vijiti viwili uwanjani mahali fulani. Anaanza kuondoka; anaenda zake uwanjani. Atazama huku na huko, "Leo, ni joto vipi!" Kilio kutoka mjini, wazurura usiku wanakuja, wakitembea kwa shida wakinywa divai zao na kadhalika. Anatazama barabarani asione kitu. Anaokota kijiti kimoja, sehemu ya msalaba, kujitolea mwenyewe. Anapata kijiti kingine, na alipokiokota kijiti hicho cha pili . . .

100 Lo, hapana shaka kulikuwa na huzuni sana, huku mauti yamekaa mlangoni. Yeye na mwanawe iliwapasa kula kipande kimoja kidogo cha mkate huo kisha wafe. Hiyo ilikuwa hiyo tu! Na wakati mwingine katikati ya huzuni ndipo tunapoisikia sauti.

101 Alipokiokota hicho kijiti cha pili kisha akaanza kurudi, sauti ikatoka upande wa pili wa lango, kasema, "Niletee maji kidogo chomboni."

102 Akageuka akaangalia huku ameshika hivi vijiti viwili mkononi mwake, huku unga umekisha kuchanganywa na mafuta na uko tayari. Alisema tayari alikuwa ameutayarisha, na kuuchanganyia. Hivyo ndivyo, Neno na Roho havina budi kuchanganywa pamoja, na kuviweka juu ya msalaba wa kujitolea kibinafsi kukanusha cho chote ambacho ni kinyume cha yale umekwisha omba. Hilo ni kweli. "Nilivichanganya; sasa naenda kuokota hivi vijiti."

Na sauti hiyo ikasema, "Niletee maji kidogo chomboni."

103 Anatazama, kisha anamwona mtu amesimama, akiegemea langoni, mwenye mashavu yaliyokonda, ana ndevu, upara, akitazama mbele ya lile lango huku amejizungushia ngozi ya kale ya kondoo. Ilionekana kama alikuwa mzee muungwana aliyeonekana kama mwenye huruma. Yeye akasema, "Nitashiriki maji yangu pamoja naye."

104 Maji ya Uzima, uko tayari kumpa mtu ye yote, kumwambia mtu ye yote, kuenda kila mahali. "Hebu kidogo, Bwana."

105 Anaanza kurudi huku ameshika vijiti mkononi mwake. Kisha ile sauti ikanguruma tena. "Hautashiriki maji yako tu, bali niletee kipande cha mkate mkononi mwako." Mkate wa

Uzima, maji ya Uzima, yalikuwa ya Uzima? Angekufa mara hayo yalipokwisha.

106 "Niletee maji yako na uniletee mkate wako." Tunaona nini hapa? Tunaweza kuona somo gani? "Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki Yake yote; mambo mengine mtaongezewa." "Niletee maji kidogo na kipande cha mkate."

107 Kisha anageuka katika huzuni yake; naweza kumsikia akisema, "Bwana!"—kitu kama hiki—"Wewe ni tofauti na watu wale nimewahi kuwaona. Na mtu ninayeweza kumsikia akinena, yaonekana una hakika sana wa yale unayosema. Bali nina unga tu wa kutosha, konzi moja tu, na kijiko kimoja tu cha mafuta. Nitautengeneza, nami nitauoka kwa hivi vijiti viwili. Nami nitaula, mimi na mwanangu, kisha tufe. Hayo tu ndiyo niliyo nayo."

108 Ni nini tunachosikia tena basi. "Bali niletee huo mkate mdogo kwanza!" Mungu kwanza! Haidhuru mtu ye yote atasema nini, yale kitu kingine cho chote, yale thibitisho lo lote, jinsi kulivyo na huzuni, hata iwe nini, mchukue Mungu kwanza, Neno Lake kwanza.

109 "Daktari alisema siwezi kupata nafuu," bali Neno Lake kwanza! "Mimi ni mwenye dhambi sana!"; "Mimi ni malaya!"; Mimi ni mcheza kamari!"; "Mimi ni mlevi!" Neno la Mungu kwanza! "Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu." Mungu kwanza.

110 "Nenda kaniletee mkate mdogo kwanza. Niletee yo yote uliyo nayo." Je, uko tayari kuyatoa mikononi Mwake?

111 Maisha yangu, yote niliyo, mimi nina umri wa miaka hamsini. "Je, uko tayari, William Branham, kuyaweka Kwangu? Mko tayari, enyi watoto wadogo kuyaweka maisha yenu Kwangu? Mko tayari? Mnaweza kufanya hivyo? Enyi wagonjwa, mnaweza kunitumaini Mimi? Niwekeni niwe wa kwanza."

112 "Niletee kipande cha mkate mkononi mwako kisha uniletee maji kidogo." Akamtazama. Kuna kitu kilichomwambia ya kwamba mtu huyo alijua alichokuwa akinena. Mungu anawajua walio Wake. Kondoo . . . "Kondoo Zangu wanaijua sauti Yangu. Wanajua kama ni Maandiko au siyo, au ni kweli au sivyo."

113 Anageuka kwa kutii. Hilo ndilo likupasalo kufanya. Naye alipogeuka apate kutii aliyoagizwa kufanya na nabii, ndipo ngurumo ikashuka kutoka Mbinguni ambayo kila mtu hutarajia kusikia. Kwa kuwa kulitokea ngurumo kutoka katika sauti ya nabii ambayo kila mwenye dhambi na kila aliye mgonjwa hutamani kusikia. "BWANA ASEMA HIVI." Jinsi tunavyotamani kuisikia.

114 Jinsi watu wanavyoketi barabarani mwangu, na kusema, "Njoo kwenye huu mlango; binti yangu hawezi, mtoto wangu

mchanga, *fulani* wangu, sema tu Neno." Wawezaje kulisema kabla halijaingia mdomoni mwako? Ungekuwa ukilisema wewe mwenyewe. Bali wao wanatamani kusikia hilo BWANA ASEMA HIVI.

115 Ndiyo hiyo ikaja kutoka kwenye ua, kwa kuwa yeye alikuwa anatii, kisha huzuni ikakatizwa: "BWANA ASEMA HIVI, Ile chupa haitaisha ama lile pipa kupungua hata siku ile Bwana atakapoleta mvua juu ya nchi." Lo, ni faraja jinsi gani.

116 Akaoka ule mkate, akampa nabii. Akarudi akaoka wake na wa mwanawe, nao wakala na kunywa wakiwa na vingi duniani. Je, ulitoka wapi? Uliingiaje mle? Hebu niambieni kisayansi ulikotoka huo unga. Hayo mafuta yalitoka wapi? Yaliingiaje mle chupani?

117 Aliyamaliza kila asubuhi; alimaliza unga pipani kila asubuhi. Nalo likawa tupu, lakini aliporudi kuchota mwingine, ulikuweko. Je, ulitoka wapi? Msadiki Mungu. Uwe na hakika na Mungu. Yeye ni Muumba.

118 Huenda ulipoteza afya yako. Huenda umepoteza ushirika wako. Lisadiki Neno Lake. Uwe na hakika ya kwamba Yeye ni Mungu. Nyakati zinazoonekana kuwa ni za huzuni huenda zisiwe za huzuni kama tu utalichukua Neno Lake na uwe na hakika ya kwamba Yeye ni Mungu.

119 Huko Ujerumani siku moja naliona picha, na daima ilidumu mawazoni mwangu. Mchoraji Mjerumani amechora ile—picha ambayo ambayo inaitwa "Nchi ya Mawingu." Na unapoiangalia ukiwa mbali, ni utusitusi wa kuchukiza sana uliopata kuona, mfungamano tu wa mawingu unapoyaangalia kutoka mbali. Bali unapoyakaribia sana, yanabadilika; ni mabawa ya malaika yanayopigapiga pamoja, wakimwimbia Bwana haleluya. Kwa hivyo hivyo ndivyo utusitusi ulivyo wakati mwingine. Ukiiangalia toka mbali, inaonekana yenye utusitusi na giza; bali mchukue Mungu kwa Neno Lake na uhakikishe ya kwamba Yeye ni Mungu, nawe usonge mbele karibu nalo; utapata ya kwamba ni mabawa ya malaika yakipigapiga pamoja.

120 Yeye alikuwa karibu na alivyokuwa Ibrahimu, aliyeitwa kutoa kila alichokuwa nacho, na kukiweka katika madhabahu ya sadaka. Labda umeitwa hivyo asubuhi ya leo; acha njia zako; acha kutokuamini kwako; acha kila kitu ulicho nacho, kisha chukua yale Mafuta na Neno uvichanganyie pamoja, kisha uviweke juu ya madhabahu ya kujitolea mwenyewe. Utatambua ya kwamba itamfanya Mungu ajitokeze jukwaani hakika kama ninavyosimama humu mimbarani.

121 Wazia hayo tunapoomba. Je, una haja leo? Je una haja iliyo kuu kuliko unavyoweza kuipata kimwili? Je, una uhaba wa pesa hivi kwamba hata hauwezi kulipia kodi ya nyumba? Je, watoto wanataka viatu vipya, na hauna pesa za kuvinunua? Je, pipa

limekauka nyumbani mwako na chupa karibu kuisha? Huwezi ukawanunulia vyakula mifugo wako, na kuna kasoro fulani, kumbuka, Yeye alitoa ahadi.

122 Je, wewe ni mgonjwa, naye daktari anasema ya kwamba unahitaji upasuaji na huna pesa za kufanya hivyo? Je, una haja?

123 Je, wewe ni mwenye dhambi? Je, mahitaji yako ni makubwa, ukijua ya kwamba Mungu akikuita leo ungepotea? Je, wewe ni mtu aliyeanguka anayemkimbia Mungu nawe unajua u mshiriki wa kanisa fulani, bali unajua hauko sahihi, dhamiri yako inakwambia kulingana na Neno kwamba wewe hauko sahihi, nawe una haja? Usiache maneno haya yakaangukie ardhi iliyo na miiba ama juu ya miamba, mioyo ya mawe; na yaangukie udongo mwema, wenye rutuba.

124 Kama u mgonjwa nawe—daktari anasema huwezi kupona, nawe unamwahidi Mungu ya kwamba utamtumikia siku zote za maisha yako, nawe una uhakika ya kwamba Yeye yu Mungu, njoo ukatimize masharti Yake. Iwapo una haja, je, waweza kujaribu kumwinulia Mungu mkono wako ya kwamba una haja ya jambo fulani? Mungu awabariki. Tuombeni.

125 Ee Bwana, kwa uhakika kama ninavyosimama katika mimbara hii asubuhi ya leo, najua ya kwamba hamna mmoja wa mikono hiyo ungaliinuliwa bila Wewe kujua, kwa kuwa Wewe ni Mungu. Ulisema, "Je! mashoromo *kadha* hawauzwi kwa senti mbili? Ninyi ni bora jinsi gani kuliko shomoro?" Ni zaidi jinsi gani ulivyoona mikono ya hao watu wanaokufa ambao Mwanao Yesu aliwafia. Ni zaidi jinsi gani ulivyoiona mikono yao kuliko jinsi ungalimwona shomoro kama angalianguka asubuhi ya leo. Nakisia kwa—mashomoro dazani moja hawangeuzwa senti moja asubuhi ya leo, kwa maana hamna mtu anayewataka; ingekuwa vigumu kuwabeba. Bali unamjua kila mmoja wao; unajua kila unyayo ulio mwilini mwao. Unajua kila unywele ulio vichwani vyetu.

126 Ee Bwana, yajibu maombi; hebu wao wawe na hakika asubuhi ya leo ya kwamba Wewe ni Mungu, na ni Roho Wako. Hebu na utusitusi na viinimacho vya dini hii ya kisasa viwaondokee wao, kule kusema, "Lo, mimi ni wa kanisa *fulani*." Mungu, hebu hilo na litoweke kutoka niani mwao sasa hivi. Katika wakati huu mmoja hebu wao na wapate tazamo la mara moja la Uzima wa Milele. Nao watautafuta na kuuonea njaa, kujua Mungu ni nani, nao wana hakika ya kwamba Yeye yuko; Yeye hutimiza Neno Lake.

127 Kwa wenye dhambi, hebu na watubu upesi, wawe tayari kwa ubatizo katika Jina la Yesu Kristo. Nawe uliahidi ya kwamba utawapa Roho Mtakatifu. Ulisema hivyo, Bwana; Nawe hutimiza ahadi Yako.

128 Huyu ni mtu aliyeanguka aliye na hakika ya kwamba Wewe ni Mungu, nao wamepotea, hebu na waje leo, kwa kuwa Wewe

ulisema, "Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu."

129 Iwapo kuna wale walio wagonjwa, hebu na watambue ya kwamba Wewe ni Mungu, unalitimiza Neno Lako; huna budi kulitimiza Neno Lako. Nao wanapokaa na Mafuta yao, Roho aliye ndani yao anayekiri wanaamini, na pia pamoja na Neno, Mkate wa Uzima uliotolewa, Kristo aliyesagwa kwa ajili yao katika Agano la Kale na katika Agano Jipya kuonyesha ya kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. . . Hebu wao na walichanganye hilo Neno na Mafuta, Roho, waliye naye, kisha wasimame kwa miguu yao madhabahuni, waseme, "Hayo ndiyo yote niliyo nayo, Bwana, nayaleta." Lo, jinsi utakavyoyazidisha, jinsi yatakavyomwita Mungu wa historia aje jukwaani; jinsi itakavyomfanya Yehova ainuke akiwa na moyo mkunjufu kwamba "Nina mtoto atakayenitii. Nimempitisha majaribuni, naye amethibitisha ya kwamba ananipenda Mimi. Yeye ana hakika ya kwamba Mimi niko." Kwa kuwa umesemwa, "Mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko, na huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii." Tujalie hayo wakati huu, tunapoyakabidhi Kwako.

130 Na sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na wale ambao wana haja ya cho chote, je, mwaweza kusimama kwa miguu yenu wanaotaka kuweka. . . Sasa, iwapo huna hakika ya kwamba Yeye ni Mungu. . . Kama una hakika Yeye ni Mungu, naye ataitimiza ahadi Yake, wokovu, uponyaji, hata iwe nini; iwapo una hakika ya kwamba Yeye ni Mungu, simama kwa miguu yako. Ikiwa una mtu mwingine unayetaka kumwombea, simama kwa miguu yako kama una—una hakika ya kwamba Yeye ni Mungu. "Haja yako na ijulikane katika kusanyiko la watakatifu. Unafanya hivyo unaposimama kwa. . . Mimi nina hakika ya kwamba Yeye ni Mungu. Ninaamini ya kwamba Yeye hulitimiza Neno Lake, nami nina hakika ya kwamba haja yangu naiweka chini ya Damu sasa hivi. Kama ukifanya hivyo weka kila dhambi, kila. . . Dhambi ni kutokuamini. Huenda ukawa mshiriki wa kanisa, bali ninamaanisha dhambi, kutokuamini kwako. Unaiweka chini kama dhabihu; unaitoa dhabihu; unakuja msalabani. Utatoa dhabihu kutokuamini kwako kwote na ukukabidhi Yeye na kujua ya kwamba Yeye yuko, nawe una hakika ya kwamba Yeye atakujibu. Ikiwa ndivyo ulivyo, inua mkono wako. Kaeni hivyo.

131 Bwana, Wewe u Mungu. Ndiyo haya Mafuta yao pamoja na Mahindi yao yaliyochanganywa pamoja; wao wanayaleta msalabani ambapo moto wa Mungu utaiangukia mioyo yao—kama kweli wao wanakusudia hilo kweli—na kuiteketeza dhabihu yao. Utajitokeza jukwaani, uabiri maji mengi. Ukija kutoka Mbingu huku umepanda gari la moto utaitikisa mbingu yote na nchi upate kuwapa hao dhawabu.

132 Wanaposimama huku mikono yao imeinuliwa juu, ikionyesha ya kwamba wao wanaamini nao wamejilaza pamoja na kila ombi walilo nalo katika madhabahu Yako. . . Ee Mungu wa Mbingu na nchi, Hakimu wa Mbingu na nchi, hakika Hakimu wa Mbingu na nchi atatenda haki; hakika atatimiza Neno Lake. Ewe uijuaye mioyo ya wanaume, mioyo ya wanawake, mioyo ya watu hawa.

133 Bwana Mungu, naiinua mikono yangu mwenyewe juu, kwa kuwa najua nina badiliko la huduma sasa. Nami naamini ya kwamba Wewe uko; nimekuona Wewe ukisimama kule katika Nguzo ya Moto. Nimekuona ukizichunguza siri za mioyo ya wanadamu, na haujakosea hata wakati mmoja. Uliiahidi ulipoifanya kule upande wa pili wa barabara hapa, ulipoanza kushughulikia na kuyafanya mambo haya. Nawe ulinikinga kila mahali duniani. Mimi nina hakika Wewe ni Mungu, nina hakika ya hilo.

134 Najitolea pamoja na watu hawa pamoja na dhabihu ya yote niliyo nayo, Bwana, Kwako kwa ajili ya utumishi. Ninaanza tena, Bwana, kuuzunguka ulimwengu. Nisaidie, Ee Mungu. Iwapo nimekosa kukuamini wakati wo wote, nisamehe dhambi zangu, nisamehe kutokuamini kwangu. Najua ya kwamba Wewe upo na huwapa mema hao wakutafutao.

135 Vivyo hivyo, nazitubu dhambi za watu wangu asubuhi ya leo, unyonge wao na kutilia shaka kwao, wanaposimama wameinua mikono yao juu. Natubu dhambi zao, Bwana, na udhaifu wetu wote. Mtume Roho Mtakatifu juu yetu pamoja na muhuri wa kibali Chako, ya kwamba Wewe ni Mungu, na uko hapa sasa kutupokea, na kutuchukua mikononi Mwako, na kutukomboa kwa kila kitu tulichopoteza. Kama ni afya yetu, na irudishwe mara mia. Kama ni nafsi yetu, na iturudie kama kitu kinachochanua na kung'aa, kimejazwa Roho Mtakatifu kipate kupelekwa mbele za Mungu. Kama ni kutokuamini, na kuturudie tena, Bwana, tukiwa na imani ya kuhamisha milima. Tujalie, Bwana.

136 Tunaamini ya kwamba Wewe unatenda kazi, Roho Mtakatifu, akilowesha kupitia jengo hili, juu ya watu hawa, na katika mioyo yao, akiwafanya wamkubali Mungu Aliye Hai. Tunafanya hili katika Jina la Yesu Kristo.

> Yesu kwa imani
> Nakutumaini,
> Peke yako;
> Nisikie sasa,
> Na kunitakasa,
> Ni Wako kabisa
> Tangu leo.

137 Mnakusudia hilo? Mnalipokea, inueni mikono yenu, mkaseme, "Sasa nalipokea kutoka Kwake."

Hapa nazunguka,
Katika mashaka,
Na matata;
Palipo na giza,
Utaniongoza,
Hivi nitaweza
Kufuata.

138 Natuinamishe vichwa vyetu. Baada ya ujumbe huu mkali na mgumu sana, ulio mjeuri na ukaletwa kwa njia ovyo, bali ni Kweli...Na iwapo utaamini kwa unyenyekevu uliyoomba upate, usiruhusu cho chote kikusukume kikuondoe katika hiyo barabara iliyo nyofu. Simama papo hapo. Haidhuru nitahubiri vipi, lo lote nitakalofanya, ama lo lote mtu ye yote angefanya, halitafanya neno hata utakapolikubali kama mali yako binafsi.

139 Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote, kila kitu ulichotamani...Kama umekwisha kutubu dhambi zako, Mungu amekusamehe. Usilitilie shaka tena! Iwapo wewe umeanguka, umerudishwa asubuhi ya leo. Iwapo unahitaji Roho Mtakatifu, basi batizwa katika Jina la Yesu Kristo upate ondoleo la dhambi zako. Hilo ni Neno la Mungu. Yeye hataligeuza kwa ajili ya kanisa lo lote, dhehebu lo lote, kwa ajili ya mtu ye yote. Halina budi kuwa hivyo. Hatuna budi kutimiza masharti Yake, si masharti ya kanisa, masharti Yake. Hivyo ndivyo itupasavyo kufanya.

140 Kama Yeye alisema kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa...Kama wewe u mgonjwa, nimekuombea ombi la imani. Umeliomba moyoni mwako na ukaamini, likubali, shikilia hilo; haina budi kuwa hivyo. Hamna kinachoweza kuichukua.

141 Haidhuru kuna utusitusi mwingi vipi...Unasema, "Vema, inaonekana kana kwamba ningali mgonjwa." Hilo hali...Ni mabawa ya Malaika yaliyowekwa pamoja. Hivyo tu. Ni Mungu katika hali ya baraka. Inaonekana kama utusitusi kwako. Ijongee karibu; kisha uiangalie tena. Uone kama si Mungu anayesimama pale akitimiza Nano Lake.

142 Sasa, huku tunapoinamisha vichwa vyetu, nitamwachia Ndugu Neville ibada, mchungaji wetu.

Uwe Na Hakika Na Mungu SWA59-0125
(Be Certain Of God)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Januari 25, 1959, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1989 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org